

Ridhiwani aagiza usalama wa mtandao, matumizi sahihi

**Na Veronica Mheta,
Arusha**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete amezigiza taasisi za serikali kutumia mifumo ya kisasa kwa usalama na usahihi ili kuhakikisha maendeleo yanakuza zaidi.

Akasisitiza maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kutumia matumizi sahihi ya mtandao ili kuchagiza maendeleo kwa

serikali ikiwemo taasisi zake kwa ujumla.

Ridhiwani aliyasema hayo wakati wa kufunga Mkutano wa Nne wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kuongeza kuwa lazima sasa serikali mtandao izingatie sheria, viwango na sera katika kubadilishana taarifa za serikali.

Alisema ustahamilivu, mageuzi na ujenzi mpya wa maridhiano ni nguzo muhimu katika uletaji chachu ya maendeleo nchini ikiwemo kuondoa changamoto za wananchi kupitia

mifumo na kuagiza taasisi za umma kusomana kupitia mifumo ya kidijiti.

Ridhiwani alisema kuna watu wanatumia barua pepe zisizo rasmi kwa ajili ya kutapeli wananchi katika aji-ra na malipo, hivyo ni lazima wataalamu wa Tehama hasa serikali mtandao kuziangalia kwa makini ili kuhakikisha usalama wa mtandao un-adhibitiwa katika matumizi sahihi ya mtandao.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kuhakikisha e-GA inafikia malengo yake katika

kuimarisha usalama zaidi wa jitihada za serikali kutoa ufanisi wa kidijiti kupitia serikali mtandao.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Benedict Ndomba alisisitiza endapo miradi ikiwa na mifumo ya Tehama, itasaidia uokoaji wa fedha za umma ikiwemo udhibiti wa fedha za serikali.

Alisema mamlaka hiyo imepokea maoni na uboresh-aji katika ufanisi wa utendaji kazi ikiwemo kuendeleza ushirikiano na utatuzi wa changamoto kwa jamii nzima

ikiwemo utoaji huduma kwa umma sanjari na kubuni na kusanifu mifumo mbalimbali ya serikali mtandao katika kuleta tija kwa wananchi.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa e-GA kutoka Serikali ya Zanzibar, Said Seif Said alipongeza ushirikiano uliopo baina ya pande hizo mbili kwa ajili ya kuhakikisha utendaji kazi maofisini unakuwa kwa kasi kubwa kupitia serikali mtandao na Tehama.

Akisoma maazimio kumi yaliifikasiwa kwenye e-GA kabla ya mwaka wa fedha.

hicho mmoja kati ya washiriki wa mkutano huo, Priscaus Kiwango alisema kila taasisi iteue ofisa Tehama mmoja atakayesimamia miongozo na kanuni za usimamizi bora wa mtandao.

Akataka taasisi za umma ziboreshwe na kutumia teknolojia ya habari mawasiliano katika utoaji huduma kwa wananchi ikiwemo kufanya tathmini ya hali ya Tehama ikiwemo uundaji wa ripoti katika kila taasisi husika kuwasilisha kwenye e-GA kabla ya mwaka wa fedha.